

Onyo: Sheria hizi zimetafsiriwa na JMT (Jumuiko la Maliasili Tanzania) – na siyo tafsiri ya kiofisi ya serikali. JMT haitahusika na uharibifu au usumbufu wowote utakaowapata au utakao mpata muhusika yeoyote kutokana na tafsiri ya sheria hizi.

TANGAZO LA SERIKALI NAMBA 196.

Limechapishwa 14 septemba 2007.

**SHERIA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI
(SHERIA NAMBA 283 R.E 2002)**

KANUNI

(Zimetungwa chini ya kifungu namba 94)

**HIFADHI YA WANYAMAPORI (MATUMIZI YA WANYAMAPORI KWA NJIA
ISIYO YA ULAJI)**

KANUNI ZA MWAKA 2007

**SEHEMU YA I
MATAMKO YA AWALI**

Kutajwa Kichwa cha habari

1. Kutajwa na Mwanzo wake
2. Kutumika
3. Tafsiri

**SEHEMU YA II
MASHARTI NA IDHINI**

4. Hairuhusiwi kutumia wanyamapori kwa njia isiyo ya ulaji bila kupata leseni au idhini.
5. Maombi ya kufanya biashara ili kutumia wanyamapori kwa njia isiyo ya ulaji.
6. Utoaji wa idhini kwa masharti.
7. Idhini maalumu.
8. Matumizi ya wanyamapori kwa njia isiyo ya ulaji katika vitalu vya uwindaji, hifadhi ya wanyama, bustani ya wanyama n.k
9. Masharti ya biashara na uwekezaji.
10. Masharti ya utafiti na shughuli za elimu.
11. Mabadiliko ya umiliki wa mwendeshaji bila kumtaarifu Mkurugenzi.
12. Kuzuia matumizi ya wanyamapori kwa njia isiyo ya ulaji bila kuwa na muongozo uliosajiliwa.
13. Hakuna kizuizi juu ya matumizi ya wanyamapori kwa njia isiyo ya ulaji.

**SEHEMU YA III
ADA**

14. Ada.
15. Tofauti, kusimamishwa au kutengua idhini.
16. Idhini ya mwenyekibali kusikilizwa.
17. Kukata rufaa kwa Waziri.

Onyo: Sheria hizi zimetafsiriwa na JMT (Jumuiko la Maliasili Tanzania) – na siyo tafsiri ya kiofisi ya serikali. JMT haitahusika na uharibifu au usumbufu wowote utakaowapata au utakao mpata muhusika ye yote kutokana na tafsiri ya sheria hizi.

MAJEDWALI

TANGAZO LA SERIKALI NAMBA 196.

Limechapishwa 14septemba 2007.

SHERIA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI,

(SHERIA NAMBA 283)

KANUNI

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 94)

HIFADHI YA WANYAMAPORI (MATUMIZI YA WANYAMAPORI KWA NJIA
ISIYO YA ULAJI) KANUNI ZA MWAKA 2007

SEHEMU YA I
MATAMKO YA AWALI

Kutajwa na
Mwanzo wake

1. Kanuni hizi zitajulikana kama za hifadhi ya wanyamapor (matumizi ya wanyamapor kwa njia isiyo ya ulaji) kanuni za mwaka 2007 na zitaanza kutumika tarehe ambayo zimechapishwa.

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika katika maeneo yote yeny wanyamapor isipokuwa katika hifadhi za taifa na eneo la hifadhi ya Ngorongoro.

Tafsiri
Sheria namba
283

3. Katika kanuni hizi isipokuwa kama itaelezwa vingine:-
“Sheria” inamaana ya sheria ya hifadhi ya wanyamapor;

“Afisa mwenye mamlaka” ina maana ni Mkurugenzi, Afisa wanyamapor, Msimamizi wa wanyamapor, Ofisa wa polisi, mwajiriwa wa hifadhi ya taifa au mwenye cheo cha juu ya mhifadhi wa wanyamapor na itahusisha maafisa ambao wameteuliwa kwa maandishi na Mkurugenzi.

- (a) Mwajiriwa wa idara ya misitu au mwenye wadhifa juu ya afisa msaidizi wa misitu;
- (b) Mwajiriwa wa idara ya uvuvi au mwenye wadhifa juu ya afisa msaidizi wa uvuvi;
- (c) Mwajiriwa wa idara ya mambo ya kale, au mwenye wadhifa juu ya mhifadhi wa mambo ya kale;
- (d) Mwajiriwa wa idara ya utalii au mwenye wadhifa juu ya afisa msaidizi wa utalii; na
- (e) Afisa ye yote wa jamii au mtu ye yote aliyeteuliwa kama inavyoonyesha kwenye maandishi na Mkurugenzi;

Onyo: Sheria hizi zimetafsiriwa na JMT (Jumuiko la Maliasili Tanzania) – na siyo tafsiri ya kiofisi ya serikali. JMT haitahusika na uharibifu au usumbufu wowote utakaowapata au utakao mpata muhusika yeoyote kutokana na tafsiri ya sheria hizi.

“Eneo la hifadhi ” inamaana:-

- (a) Pori la akiba lililoanzishwa chini ya kifungu cha 5 cha sheria hii;
- (b) Eneo la pori tengefu lililoanzishwa chini ya kifungu cha 6 cha sheria hii;
- (c) Hifadhi ya taifa iliyoanzishwa chini ya sheria ya hifadhi ya taifa;
- (d) Eneo la hifadhi ya Ngorongoro lililoanzishwa chini ya sheria ya hifadhi ya Ngorongoro;
- (e) Hifadhi ya msitu iliyoanzishwa chini ya sheria ya misitu;
- (f) Maeneo ya hifadhi ya wanyamapori yaliyoanzishwa chini ya sheria ya hifadhi ya wanyamapori;

Sheria Namba
14
ya mwaka 2002

“Msimu uliotengwa kwa shughuli maalumu” inaamanisha kipindi ambacho kimetangazwa na waziri chini ya sheria;

“Maeneo ya utamaduni” inaamanisha maeneo ambayo yana thamani ya kiutamaduni na hadhi ya uzuri wa kipekee;

“Mkurugenzi” inamaana Mkurugenzi wa wanyamapori aliyeuleliwa chini ya sheria hii;

“Maeneo yenye mahema” inamaana mahema yenye miundo iliyoendelezwa kwa lengo la kutoa huduma za kimsingi za mahema;

“Eneo mtawanyiko” Ina maana eneo ambalo kwa mazoea linatumika na wanyamapori kwa lishe, kutaga au kuhifadhi mayai au kutunza watoto na pamoja na sehemu ya kuzalia;

“filamu” kitendo cha kuchukua mfululizo wa taswira ya vitu mbalimbali kwa kutumia kamera ili kutoa picha halisi ya kitu kinachotembea mfululizo au utaratibu maalumu wakati kivuli chake kikionyeshwa kwenye kioo (skrini);

“Kuweka mahema ya muda” ina maana eneo la mahema ambalo limewekwa kwa muda na watalii mbali kidogo kutoka kwenye eneo la kudumu la mahema;

“eneo la kuhifadhi wanyamapori” ina maana eneo ambapo wanyamapori wanahifadhiwa katika sehemu maalumu, hususani katika eneo kubwa katika hali ya asili kwa lengo la elimu na burudani;

“ardhi ya jumla” ina maana ardhi yote ya jamii ambayo ina wanyamapori ambayo haijahifadhiwa au ardhi ya kijiji kama ilivyoelezwa kwenye sheria;

“mgeni” ina maana mtu yeoyote ambaye analipa kiwango fulani cha pesa kama malipo hayo yamefanywa na mtu huyo au na mtu mwingine yeoyote, mwenye kutwaa au hifadhi kwa makazi, makazi katika nyenzo za utalii;

“mwongozaji” ni mtu anayeambatana na wageni au mtalii katika shughuli za utalii ambaa haulengi kuwinda wanyama;

“kitalu cha uwindaji” ina maana eneo lolote ambalo lina wanyamapori ambalo limetengwa na kuidhinishwa na Mkurugenzi kwa ajili ya

Sheria namba
283

Onyo: Sheria hizi zimetafsiriwa na JMT (Jumuiko la Maliasili Tanzania) – na siyo tafsiri ya kiofisi ya serikali. JMT haitahusika na uharibifu au usumbufu wowote utakaowapata au utakao mpata muhusika ye yeyote kutokana na tafsiri ya sheria hizi.

uwindaji ili kuweza kupata nyara;

- “nyumba ya wageni” ina maana huduma ya makazi kwenye jengo imara la kudumu lililotengenezwa kwa saruji au mbaou au kitu chochote kilichotengenezwa kwa lengo la kutoa makazi kwa watalii lenye uwezo wa vitanda zaidi ya 24 na ambavyo havizidi vitanda 75;
- “njia za wahamaji” ina maana eneo la ukanda au eneo maalumu linalotumiwa na kundi la wanyamapori wakati wa mzunguko wa kuhama au msimu maalumu;
- “Waziri” ina maana Waziri mwenye dhamana ya mambo yanayohusiana na uhifadhi wa wanyamapori;
- “uendeshaji wa kuangalia wanyama usiku” ina maana shughuli ya kuendesha gari au boti kipindi ambapo jua limezama mpaka saa 3:00 usiku kwa lengo la kungalia wanyamapori kunakofanywa na watalii;
- “idhini ya kutumia wanyamapori kwa njia isiyo ya ulaji” ina maana mamlaka aliyonayo Mkurugenzi ya kufanya shughuli za utalii ambaou siyo ya ulaji wa wanyamapori;
- “Eneo la wazi” ina maana eneo lolote ambalo lina wanyamapori licha ya hifadhi ya taifa, eneo la hifadhi ya Ngorongoro, pori tengefu, pori la akiba, meneo ya jamii ya kuhifadhi wanyamapori, bustani ya wanyama, shamba la wanyama, hifadhi ya wanyama na ranchi za wanyamapori;
- “mtekelezaji” ina maana mtu yeyote ambaye ana miliki/kutekeleza au kuendesha nyenzo za utalii au anahuksika kusimamia nyenzo hizo;
- “mwongozaji mzoefu” ni mwongozaji wa safari aliyesajiliwa ili kuongoza shughuli za matumizi ya wanyamapori kwa kutokuwala;

- “safirisha kwa boyo” ina maana mapumziko ya nje yanayofanywa kwa kuelea juu ya maji kwa kutumia boyo;
- “eneo la mahema maalumu” ina maana eneo ambalo halina nyenzo zinazotumika kwa ajili ya kupiga kambi;
- “uvuvi wa kimichezo/burudani” ina maana shughuli za uvuvi kwa ajili ya burudani;
- “kambi ya mahema” ina maana nyenzo za malazi/makazi ambazo siyo za kudumu kwa lengo la kuwapa makazi watalii lenyo uwezo wa vitanda visivyozidi 24;
- “utalii” ina maana shughuli za mtu kusafiri kwenda sehemu nyingine tofauti na mazingira yake ya kawaida kwa masaa zaidi ya 24 na kipindi kisicho zidi mwaka mmoja kwa lengo la kufanya shughuli maalumu katika sehemu ambayo inatembelewa, pale ambapo shughuli hii inafanywa na mkazi itajulikana kama utalii wa ndani;
- “mtalii” ina maana mtu yeyote ambaye anasafiri kwenda sehemu nyingine tofauti na mazingira yake ya kawaida kwa masaa zaidi ya 24 na kipindi kisicho zidi mwaka mmoja kwa lengo la kufanya shughuli maalumu katika sehemu ambayo anatembelea;
- “mwongozaji wa asili” ni mtu ambaye ana ujuzi wa asili wa uongozaji wa shughuli za wanyamapori, elimu ya asili au maarifa ambaye anafuatana na watalii katika kutekeleza shughuli za matumizi ya wanyamapori bila kuwala;

Onyo: Sheria hizi zimetafsiriwa na JMT (Jumuiko la Maliasili Tanzania) – na siyo tafsiri ya kiofisi ya serikali. JMT haitahusika na uharibifu au usumbufu wowote utakaowapata au utakao mpata muhusika yeote kutokana na tafsiri ya sheria hizi.

“mgeni” ina maana mtu yeote ambaye sehemu yake ya makazi ya kawaida ni nje ya sehemu ambayo imetembelewa kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja kwa sababu zingine zaidi ya kuajiriwa;

“sakafu ya wanyamapor” ina maana ni eneo la ardhi ambalo linatumwa na wanyamapor wa aina mbalimbali katika kipindi ambapo wanasaferi kutoka eneo moja la kiikolojia kwenda eneo lingine ili kuweza kupata mahitaji yao ya msingi;

“ufugaji wa wanyamapor” ina maana ufugaji makini wa wanyamapor, uzalishaji wa aina moja au zaidi wa wanyamapor katika eneo lililofungwa ambalo lina ukubwa wa hekta zisizo zidi ishirini na tano kwa njia ambayo ina lengo la kufuga wanyama na mtazamo wa kujishughulisha katika njia tofauti za kutumia wanyamapor;

“ranchi ya wanyamapor” ina maana eneo lililozungushiwa au kutozungushiwa ua ambalo lina wanyamapor ambao wanatumika kwa kiwango kikubwa kwa njia tofauti ambapo njia mbalimbali za ziada za kusimamia wanyamapor zinatumika ili kuwazuia wanyama hao kutangamana, ikiwa ni pamoja na uwindaji wa kimichezo, uvunaji, uuzaji wa wanyama waliohai, utalii na uvuvi;

“bustani ya wanyamapor” ina maana ni eneo ambalo wanyamapor wanahifadhiwa katika mazingira ya asili kwa lengo la burudani, utafiti na mambo ya elimu;

SEHEMU YA II

MASHARTI NA IDHINI

Hairuhusiwi
kutumia
wanyamapor
kwa njia ya ulaji
bila kuwa na
leseni au kibali

Maombi ya
shughuli za
matumizi ya
wanyamapor
kwa lengo la
kutokuwala

Utoaji wa idhini
kwa masharti

4. Mtu yeote haruhusiwi kujishughulisha na matumizi ya wanyamapor kwa njia isiyo ya ulaji katika eneo lolote, isipokuwa kama amepata idhini chini ya sheria hizi.

5.-(1) Mtu yeote mwenye nia ya kufanya uwekezaji kwa njia ya kujenga kambi ya mahema au nyumba ya wageni, kufanya biashara, utafiti na shughuli za elimu katika matumizi ya wanyamapor bila kuwala atatuma maombi kwa Mkurugenzi kwa utaratibu uliowekwa kwenye jedwali la kwanza la kanuni hizi.

(2) Kutokana na kanuni ndogo (1), Mtu yeote hataruhusiwa kufanya matumizi ya wanyamapor kwa lengo la kutokuwala bila kuwa na leseni iliyotolewa na sheria ya leseni ya wakala wa utalii au leseni yoyote inayoruhusu mwenye leseni kutekeleza shughuli au biashara yoyote ya utalii kutoka kwa Mkurugenzi wa utalii.

6.-(1) Mkurugenzi anaweza kutoa idhini ya matumizi ya wanyamapor kwa lengo la kutokuwala kwa muombaji kwa muda na masharti maalumu baada ya malipo ya ada kufanyika kama ilivyoelezwa chini ya sheria hizi.

(2) Idhini ya matumizi ya wanyamapor kwa lengo la kutokuwala iliyotolewa na Mkurugenzi chini ya sheria ndogo (1) itakuwa halali tu kulingana na maeneo na muda kama ilivyoelezwa kwenye idhini.

Onyo: Sheria hizi zimetafsiriwa na JMT (Jumuiko la Maliasili Tanzania) – na siyo tafsiri ya kiofisi ya serikali. JMT haitahusika na uharibifu au usumbufu wowote utakaowapata au utakao mpata muhusika yeoyote kutokana na tafsiri ya sheria hizi.

Idhini maalumu

Matumizi ya wanyamapori kwa kutokuwala katika hifadhi ya wanyama, bustani ya wanyama, n.k

Masharti ya biashara na uwekezaji

Masharti ya utafiti na shughuli za elimu

Kubadili umiliki wa mwendeshaji bila kumtaarifu Mkurugenzi

7. Mkurugenzi anaweza, kama kuna maombi na kama akiafikiana na waziri kutoa idhini maalumu kwa mtu mmoja au kundi la watu kwa matumizi ya wanyamapori kwa kutokuwala zaidi ya shughuli zilizoelezwa katika kanuni ya 5.

8.-(1) Mkurugenzi anaweza, kama kuna maombi kutoa idhini kwa wamiliki wa hifadhi ya wanyama, bustani ya wanyama, shamba la wanyama, ranchi ya wanyamapori na uanzishaji wowote uliosawia kufanya matumizi ya wanyamapori kwa kutokuwala.

(2) Mtu yeoyote ambaye amepewa idhini chini ya sheria ndogo (1) ya sheria namba 8 atawajibika kulinda mazingira yanayozunguka dhidi ya uchafuzi wa mazingira ambao unaweza kuhtarisha uimara wa ikolojia katika eneo husika.

9. Kulingana na sheria ya 6 na 8, mwombaji wa shughuli za biashara au uwekezaji atatahitajika:-

- (a) Kuwa na kampuni iliyosajiliwa na mamlaka halali na yenye kuaminika nchini Tanzania;
- (b) Kuwa na kiwanja chenye ofisi;
- (c) Kuwa na uwezo wa kufanya biashara ya matumizi ya wanyamapori kwa njia ya kutokuwala;
- (d) Kukubaliana na mpango wa jumla wa usimamizi wa eneo husika;
- (e) Kupata idhini ya tathmini ya athari za kimazingira kutoka kwa mamlaka husika pale inapobidi;
- (f) Kusaini makubaliano na Mkurugenzi juu ya taratibu za kumiliki vitega uchumi na uendeshaji wake;
- (g) Kulipa ada kama ilivyoolekezwa na Mkurugenzi na
- (h) Kukubaliana na masharti yoyote kama ilivyoolekezwa na Mkurugenzi.

10. Kulingana na sheria ya 7 na 8, mwombaji kwa shughuli za utafiti au shughuli za elimu anapaswa kuwasilisha kwa Mkurugenzi:-

- (a) Idhini ya utafiti kutoka kwa mamlaka husika;
- (b) Andiko la utafiti;
- (c) Barua ya utambulisho kutoka kwa taasisi ya elimu inayotambulika nchini Tanzania; na
- (d) Mara baada ya kumaliza shughuli za utafiti, kuwasilisha matokeo ya tafiti, taarifa na vielelezo kwa Mkurugenzi na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori nchini Tanzania.

11. -(1) Mtu yeoyote hataruhusiwa kuhamisha sehemu kubwa ya hisa ya umilikaji wa kampuni katika mapori tengefu bila kumtaarifu Mkurugenzi madhumuni ya kufanya hivyo.

(2) Mmilikaji mpya wa kampuni atatahitajika kukubaliana na muda na masharti ya umilikaji kama ilivyoolekezwa katika sheria hizi.

Onyo: Sheria hizi zimetafsiriwa na JMT (Jumuiko la Maliasili Tanzania) – na siyo tafsiri ya kiofisi ya serikali. JMT haitahusika na uharibifu au usumbufu wowote utakaowapata au utakao mpata muhusika yeyote kutokana na tafsiri ya sheria hizi.

Mipaka juu ya matumizi ya wanyamaporini kwa kutokuwala bila kuwa na mwongozo

Hakuna kizuizi juu ya matumizi ya wanyamaporini kwa njia ya kutokuwala

Ada

12.-(1) Mtu yeyote au kundi la watu wanaofanya matumizi ya wanyamaporini bila kuwala wataambatana na mwongozaji aliyesajiliwa ambaye:-

- (a) Ana cheti katika usimamizi wa wanyamaporini kutoka katika taasisi inayotambulika; na
- (b) Ana sifa nyingine yoyote kama ilivyoainishwa katika sheria zozote zingine zilivyoandikwa.

13. Mtu yeyote anayefanya bishara ya matumizi ya wanyamaporini kwa kutokuwala katika eneo husika atahakikisha ya kwamba utendaji wake unafanyika kwa usalama na yamkini hautazuia mamlaka zingine au mtu mwenye leseni au mtu mwininge yeyoye kupita au kufanya shughuli za kihalali kisheria au shughuli za biashara.

SEHEMU YA III ADA

14.-(1) Kila shughuli itakayofanyika katika mapori tengefu, mapori ya akiba, maeneo ya jamii ya kuhifadhi wanyamaporini na maeneo ya wazi nje ya eneo la hifadhi ya Ngorongoro na yale yaliyo chini ya TANAPA, kama ilivyoelezwa katika sheria hizi atatozwa ada kwa maelekezo ya Mkurugenzi.

(2) Bila kuleta madhara kwa sheria ndogo (1), jedwali la Tatu na Nne la sheria hizi litakuwa na athari kulingana na shughuli ambazo zimeainishwa hapa chini:-

- (a) Kuingia kwa mtu yeyote
- (b) Upigaji picha wa kibashara, filamu, au uandaaji wa nyaraka katika mapori tengefu;
- (c) Maalumu, uanzishwaji wa maeneo ya mahema, na mahema yasiyo ya kudumu katika mapori tengefu;
- (d) Kuingia kwa magari, boti zenye mashine, chelezo, mtumbwi na chombo chochote kinachoendeshwa kwa mashine au chombo kizito katika mapori tengefu;
- (e) Safari za kutembea katika mapori tengefu
- (f) Safari za kuangalia wanyama nyakati za usiku katika mapori tengefu
- (g) Uvubi wa kimichezo katika mapori tengefu
- (h) Ulinzi kwa safari za kitalii katika mapori tengefu;
- (i) Utuaji wa ndege na Maputo makubwa katika mapori tengefu;
- (j) Hifadhi ya wanyamaporini na haki ya mtumiaji

(3) Safari za usiku za kuangalia wanyamaporini zitafanyika kati ya kipindi cha machweo (kipindi jua linapozama) mpaka saa 3:00 usiku tu.

Onyo: Sheria hizi zimetafsiriwa na JMT (Jumuiko la Maliasili Tanzania) – na siyo tafsiri ya kiofisi ya serikali. JMT haitahusika na uharibifu au usumbufu wowote utakaowapata au utakao mpata muhusika ye yeyote kutokana na tafsiri ya sheria hizi.

(4) Mtu yeyote ambaye atashindwa kulipa ada yoyote kati ya kipindi kilichoelezwa chini ya sheria hizi atatakiwa kulipa nyongeza ya asilimia kumi ya ada ndani ya siku kumi na nne tangu ataarifiwe.

(5) Mtu yeyote ambaye atashindwa kukubaliana na mahitaji ya sheria ndogo (4) ndani ya kipindi kilichoelezwa atatakiwa kulipa nyongeza ya asilimia thelethini ya ada iliyoelezwa ndani ya siku kumi na nne tangu ataarifiwe.

(6) Mtu yeyote ambaye atashindwa kukubaliana na mahitaji ambayo yameainishwa katika kifungu kidogo cha (5) atakuwa na makosa na adhabu yake itakuwa ni kifungo kwa kipindi kisicho zidi miezi sita.

(7) Kwa nyongeza ya hukumu iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (5), mahakama itaamuru malipo ya ada yafanyike chini ya kifungu kidogo cha (4).

SEHEMU YA IV MABADILIKO, KUSIMAMISHWA AU KUTANGUA IDHINI

Mabadiliko,
Kusimamishwa
au Kutangua
idhini.

15.-(1) Mkurugenzi anaweza, kama itadhihirika ya kwamba mwendeshaji amevunja sheria au tamko lolote la sheria katika sheria hizi, kutangua, kusimamisha au kubadilisha idhini yoyote au masharti ya idhini ambayo yametolewa kwa muhusika chini ya sheria hizi.

(2) Ambapo Mkurugenzi atatangua, kusimamisha au kubadilisha idhini yoyote iliyotolewa chini ya sheria hizi atamtaarifu muhusika mwenye idhini kwa maandishi akieleza sababu za kuchukua maamuzi hayo.

Mwenye idhini
kusikilizwa

16.-(1) Mwenye idhini ata, ndani ya siku thelathini, kuwa na haki baada ya kupata taarifa chini ya kanuni ya 13 kuonyesha sababu ndani ya siku thelathini kwa Mkurugenzi kwa nini idhini isifanyiwe mabadiliko au kutenguliwa.

(2) Mkurugenzi ata, ndani ya siku sitini, mara baada ya kupokea malalamiko atafikiria upya au kukataa malalamiko hayo.

Kukata rufani
kwa Waziri

17.-(1) Mtu ambaye atakerwa na maamuzi ya Mkurugenzi chini ya kanunia ya 16 ya sheria hizi anaweza, ndani ya siku thelathini baada ya kupata taarifa kutoka kwa Mkurugenzi kukata rufani kwa waziri.

Makosa na
adhabu

18. Isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo, mtu ambaye atakuwa amevunja sheria ya kanuni hizi atakuwa ametenda makosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua kiasi cha shilingi milioni moja au kifungo kisichopngua miezi sita au vyote viwili kwa pamoja.

Onyo: Sheria hizi zimetafsiriwa na JMT (Jumuiko la Maliasili Tanzania) – na siyo tafsiri ya kiofisi ya serikali. JMT haitahusika na uharibifu au usumbufu wowote utakaowapata au utakao mpata muhusika yeoyote kutokana na tafsiri ya sheria hizi.

JEDWALI LA KWANZA

(Zimetungwa chini ya kanuni Namba 5(1))

HIFADHI YA WANYAMAPORI (MATUMIZI YA WANYAMAPORI KWA NJIA ISIYO YA ULAJI) KANUNI ZA MWAKA, 2007

FOMU YA MAOMBI YA IDHINI YA MATUMIZI YA WANYAMAPORI BILA KUWALA

1. Jina la mwombaji.....
2. Anuani ya posta.....
S.L.P.....
Namba ya simu ya ofisini.....Simu ya mkononi.....
Namba ya Telefax
3. Anuani (Kama ni tofauti na ya hapo juu).....
4. Hati ya kusajiliwa Kampuni namba.....
5. Nambari ya mlipa kodi.....
6. Jina, Utaifa na Umri wa wanahisa/Wakurugenzi na idadi ya hisa zilizopo.

Jina	Utaifa	Umri	Idadi ya hisa
(a).....
(b).....
(c).....
(d).....
7. Rasilimali zinazomilikiwa na mwombaji/waombaji
 - (a) Vifaa/Vyombo.....
 - (b) Magari.....
 - (c) idadi ya waajiriwa.....
 - (i) Wenye ujuzi.....
 - (ii) Wasio na ujuzi.....
 - (iii) Wa kigeni.....
 - (iv) Wenyiji.....
8. Aina ya biashara.....
9. Eneo/Maeneo ya utendaji.....
10. Muda ambao idhini inaombwa.....
11. Hadhi ya maombi-mapya/marudio
12. Sisi/Mimi tunatamka/ninatamka ya kwamba maelezo ya hapo juu ni kweli na sahihi katika nyanja zote na muombaji ataheshimu na kutii sheria za wanyamaporu na kanuni zake nchini Tanzania.

Sahihi na muhuri wa ofisi.....Tarehe.....

Kwa matumizi ya ofisi tu

Muombaji ameidhinishwa/hajaidhinishwa.....
Kama hajaidhinishwa elezea sababu
.....
Sahihi na muhuri wa ofisi.....Tarehe.....
.....

Onyo: Sheria hizi zimetafsiriwa na JMT (Jumuiko la Maliasili Tanzania) – na siyo tafsiri ya kiofisi ya serikali. JMT haitahusika na uharibifu au usumbufu wowote utakaowapata au utakao mpata muhusika ye yeyote kutokana na tafsiri ya sheria hizi.

Angalizo: Maombi yaambatane na picha tatu za ukubwa wa passport kwa kila Mkurugenzi/Mwanahisa, nakala ya hati ya usajili wa kampuni, nakala ya makubaliano na maelezo ya kisheria ya chama na namba ya utambulisho ya mlipaji kodi.

JEDWALI LA PILI

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 6(1))

HIFADHI YA WANYAMAPORI (MATUMIZI YA WANYAMAPORI KWA NJIA ISIYO YA ULAJI) KANUNI ZA MWAKA, 2007

IDHINI YA MATUMIZI YA WANYAMAPORI KWA NJIA ISIYO YA ULAJI

HAIAMISHIKI

Sehemu iliyotolewa:..... Tarehe iliyotolewa..... Tarehe ya kwisha muda wake:.....

Imetolewa kwa:.....

Mwenye anuani:.....

Idhini kwa (aina ya utalii na shughuli)

.....

Mahali

.....

Sharti jingine lolote (kama lipo):.....

.....
.....
.....

Jina na sahihi ya mwenye idhini au
Mkurugenzi wa kampuni

Jina na sahihi ya Mkurugenzi wa wanyamapor
(Bandika muhuri wa ofisi)

Onyo: Sheria hizi zimetafsiriwa na JMT (Jumuiko la Maliasili Tanzania) – na siyo tafsiri ya kiofisi ya serikali. JMT haitahusika na uharibifu au usumbufu wowote utakaowapata au utakao mpata muhusika ye yote kutokana na tafsiri ya sheria hizi.

JEDWALI LA TATU

(Zimetungwa chini ya kanuni ya 14(2))

ADA YA MATUMIZI YA WANYAMAPORI KWA NJIA ISIYO YA ULAJI

A: ADA YA KIINGILIO KWA MTU BINAFSI

(i) MAPORI TENGEFU YA SELOUS, IKORONGO, GRUMETI NA MASWA

Umri	Ada kwa mtu mmoja kwa siku moja	
	Raia (Shilingi za Tanzania) Kwa masaa 24	Wageni (Dola za Kimarekani) Kwa masaa 24
(a) Umri wa miaka 18 na kuendelea	5,000.00	50.00
(b) Umri kati ya miaka 5 mpaka 17	3,000.00	30.00
(c) Umri chini ya miaka 5	Bure	Bure

(ii) MAPORI TENGEFU MENGINE

Umri	Ada kwa mtu mmoja kwa siku moja	
	Raia (Shilingi za Tanzania) Kwa masaa 24	Wageni (Dola za Kimarekani) Kwa masaa 24
(a) Umri wa miaka 18 na kuendeklea	2,000.00	30.00
(b) Umri kati ya miaka 5 mpaka 17	1,000.00	15.00
(c) Umri chini ya miaka 5	Bure	Bure

B: ADA YA FILAMU AU UPIGAJI PICHA WA SINEMA

(ii) Filamu/Upigaji picha wa sinema

Kipindi cha utekelezaji	Ada kwa mtu mmoja kwa siku moja	
	Raia Dola za Kimarekani	Non-Citizen Dola za Kimarekani
Siku moja mpaka siku 89	50.00	200. 00
Siku 90 mpaka siku 179	40.00	150.00
Siku 180 mpaka siku 720	30.00	100.00

* Ada ya filamu/upigaji picha za cinema inajumuisha ada ya kuingilia, kupiga kambi na ada ya kuandaa filamu.

Onyo: Sheria hizi zimetafsiriwa na JMT (Jumuiko la Maliasili Tanzania) – na siyo tafsiri ya kiofisi ya serikali. JMT haitahusika na uharibifu au usumbufu wowote utakaowapata au utakao mpata muhusika ye yote kutokana na tafsiri ya sheria hizi.

C: ADA YA MAKAMBI YALIYOANZISHWA, MAALUMU AU MAKAMBI YA MUDA KATIKA MAPORI TENGEFU

(i) Eneo la makambi yaliyoanzishwa

Umri	Ada kwa mtu mmoja kwa siku moja	
	Raia Shilingi za Kitanzania	Wageni Dola za Kimarekani
(a) Umri wa miaka 18 na zaidi	5,000.00	30.00
(b) Umri kati ya miaka 5 mpaka 17	3,000.00	20.00
(c) Umri chini ya miaka 5	Bure	Bure

(ii) MAKAMBI MAALUMU/YA MUDA

Umri	Ada kwa mtu mmoja kwa siku moja	
	Raia Shilingi za Kitanzania	Wageni Dola za Kimarekani
(a) Umri wa miaka 18 na zaidi	10,000.00	50.00
(b) Umri kati ya miaka 5 mpaka 17	5,000.00	30.00
(c) Umri chini ya miaka 5	Bure	Bure

D: ADA ZA MAGARI, BOTI ZENYE MASHINE, CHELEZO NA MITUMBWI KATIKA MAPORI TENGEFU

(i) Magari

Aina ya uzito	Ada ya kuingiza gari (malipo kwa siku)	
	Usajili wa ndani	Usajili wa nje
	Shilingi za Kitanzania	Dola za Kimarekani
Uzito wa Kg 2,000	20,000.00	50.00
Uzito kati ya Kg 2,000 - 3,000	50,000.00	150.00
Uzito kati ya Kg 3,000 - 7,000	100,000.00	300.00
Uzito kati ya Kg 7,001-10,000	500,000.00	500.00

(ii) Ada ya boti za mashine

Ada ya kuingiza boti/kutembea na boti kwa siku moja	Usajili wa ndani Shilingi za kitanzania	Usajili wa nje Dola za Kimarekani
Nguvu ya boti kati ya 5-15 (5-15 HP)	100,000.00	150.00
Nguvu ya boti kati ya 16-45 (16-45 HP)	150, 000.00	200.00
45 – 50*	200, 000.00	300.00

* Boti zenye machine zenye nguvu zaidi ya 50 HP haziruhusiwi

Onyo: Sheria hizi zimetafsiriwa na JMT (Jumuiko la Maliasili Tanzania) – na siyo tafsiri ya kiofisi ya serikali. JMT haitahusika na uharibifu au usumbufu wowote utakaowapata au utakao mpata muhusika ye yote kutokana na tafsiri ya sheria hizi.

(iii) *Ada ya kuendesha chelezo/mtumbwi

Uwezo wa kuchukua abiria	Malipo kwa siku (Dola za Kimarekani)
Abiria 1mpaka watu 5	500.00
Zaidi ya watu 5 lakini wasizidi watu 10	1000.00

* Ada za kuendesha chelezo/mtumbwi ni pamoja na ada za kuingilia, ada ya kupiga kambi itatozwa tofauti kutokana na viwango vya kawaida vilivyowekwa.

E: ADA KWA AJILI YA MATEMBEZI YA SAFARI

Kundi	Malipo ya ada kwa kundi moja kwa siku moja	
	Raia Shilingi za Kitanzania	Wageni Dola za Kimarekani
Mtu 1 mpaka watu 5	50,000.00	150.00
Watu 6-10	150,000.00	500.00

F: ADA KWA AJILI YA KUENDESHA USIKU KUANGALIA WANYAMA

Umri	Ada kwa usiku mmoja	
	Raia Shilingi za Kitanzania	Wageni Dola za Kimarekani
Watoto (Umri kati ya miaka 5 mpaka 17)	20,000.00	50.00
Watu wazima (Umri kuanzia miaka 18 na zaidi)	50,000.00	100.00

G: ADA KWA AJILI YA UVUVI WA KIMICHEZO/BURUDANI

Aina ya haki ya mtumiaji	Ada	
	Raia Shilingi za Kitanzania	Wageni Dola za Kimarekani
Kuvua na kuwaacha samaki (kwa siku moja)	10,000.00	50.00
Kuvua na kuwachukua samaki (kwa samaki mmoja)	5,000.00	10.00

H: ADA ZA KUONGOZA (WATALII) KATIKA MAPORI TENGEFU

(i) Ada kwa waongozaji walioajiriwa na Serikali

Aina ya shughuli ya kitalii	Ada (Kiwango cha siku kwa Muongozaji)	
	Raia Shilingi za Kitanzania	Wageni Dola za Kimarekani
Kuendesha kuona wanyama	30,000.00	40.00
Kutembea/Kuendesha boti/Kuendesha chelezo/safari za	25,000.00	25.00

Onyo: Sheria hizi zimetafsiriwa na JMT (Jumuiko la Maliasili Tanzania) – na siyo tafsiri ya kiofisi ya serikali. JMT haitahusika na uharibifu au usumbufu wowote utakaowapata au utakao mpata muhusika ye yote kutokana na tafsiri ya sheria hizi.

mtumbwi		
---------	--	--

(ii) Ada kwa waongozaji wenyе taaluma

Ada ya usajili ya mwongozaji	*Ada ya kila siku	**Ada ya mwaka mmoja
Raia (Shilingi za Kitanzania)	20,000.00	500,000.00
Mgeni (Dola za Kimarekani)	30.00	5,000.00

* Mwongozaji ambaye siye mwajiriwa wa kambi/nyumba ya wageni/hoteli iliyopo kwenye hifadhi

**Mwongozaji ambaye ni mwajiriwa wa kambi/nyumba ya wageni/hoteli iliyopo kwenye hifadhi

I: ADA YA KURUKA KWA NDEGE NA PUTO KUBWA KATIKA PORI TENGEFU

(i) Ada ya kutua kwa ndege

Uwezo wa ndege	Ada ya kutua kwa ndege (ni pamoja na helikopta)	
	Usajili wa ndani (Shilingi za Kitanzania)	Usajili wa nje (Dola za Kimarekani)
Abiria 1 mpaka 4	25,000.00	100.00
Abiria 5 mpaka 12	30,000.00	150.00
Abiria 13 na zaidi	40,000.00	300.00

(ii) Gharama ya uwanja wa ndege

Aina	Ada inayolipwa kwa mtu mmoja kwa kutua
Mgeni (Dola ya Kimarekani)	5
Mwenyeji (Shilingi ya Kitanzania)	5000

* Malipo kwa mtu mmoja anayetua katika pori tengefu lakini anayekaa katika makambi ya mahema/nyumba za wageni nje ya pori tengefu.

(iii) (a) Ada ya uendeshaji wa puto kubwa

Uwezo wa puto kubwa	Ada kwa muda wa uendeshaji (Dola za Kimarekani)
Mpaka siku 90	3,000.00
Mpaka siku 180	6,000.00
Mpaka siku 360	9,000.00

(b) Ada ya kuruka kwa puto kubwa

Uwezo wa puto kubwa	Ada inayolipwa kwa mtu mmoja kwa kutua (Dola za Kimarekani)
Mpaka abiria 4	50.00

Onyo: Sheria hizi zimetafsiriwa na JMT (Jumuiko la Maliasili Tanzania) – na siyo tafsiri ya kiofisi ya serikali. JMT haitahusika na uharibifu au usumbufu wowote utakaowapata au utakao mpata muhusika yeote kutokana na tafsiri ya sheria hizi.

Abiria kati ya 5 mpaka 12	40.00
Abiria 13 au zaidi	30.00

J: ADA YA KUHIFADHI WANYAMAPORI NA ADA YA HAKI YA MTUMIAJI WA WANYAMAPORI

(i) Ada ya kuhifadhi wanyamapor

Aina	Ada kwa mtu mmoja kwa usiku mmoja
Kambi ya mahema/Nyumba ya wageni katika pori tengefu	25
Kambi ya mahema/nyumba ya wageni nje ya pori tengefu	15

Kampuni inayofanya kazi katika pori tengefu itaweka kiwango cha chini cha pesa cha dola za Kimarekani zipatazo 36,000 ambazo hazitarejeshwa kama ada ya uhifadhi kwa mwaka, ada italipwa wakati wa kuingia kwa mkataba (maridhiano baina ya pande mbili); siku 90 tangu tarehe ya ujenzi wa kambi ukamilike, na tarehe **1/July/** ya kila mwaka, wakati kambi/nyumba ya wageni zinatumika.

* Malipo mengine na taratibu za malipo zitakuwa kama zilivyo kwenye makubaliano kati ya serikali na mwekezaji husika.

JEDWALI LA NNE

(Zimetungwa chini ya kanuni ya 14)

ADA YA KUTUMIA WANYAMAPORI KWA NJIA ISIYO YA ULAJI KATIKA PORI LA AKIBA, ENEO LA JAMII LA KUHIFADHI WANYAMAPORI NA ENEO LA WAZI.

A: ADA YA KUANGALIA WANYAMAPORI

(1) PORI LA AKIBA NA ENEO LA JAMII LA KUHIFADHI WANYAMAPORI

Umri	Kiwango cha chini cha ada cha kuangalia wanyamapor kwa siku moja	
	Raia (Shilingi za Kitanzania) Kwa masaa 24	Mgeni (Dola za Kimarekani) Kwa masaa 24
(a) Miaka 18 na zaidi	1,000.00	20.00
(b) Miaka 5 mpaka 17	500.00	10.00
(c) Umri chini ya miaka 5	Bure	Bure

(2) ENEO LA WAZI

Umri	Kiwango cha chini cha ada cha kuangalia wanyamapor kwa siku moja	
	Raia (Shilingi za Kitanzania) Kwa masaa 24	Mgeni (Dola za Kimarekani) Kwa masaa 24
(a) Miaka 18 na zaidi	Bure	10.00

Onyo: Sheria hizi zimetafsiriwa na JMT (Jumuiko la Maliasili Tanzania) – na siyo tafsiri ya kiofisi ya serikali. JMT haitahusika na uharibifu au usumbufu wowote utakaowapata au utakao mpata muhusika ye yote kutokana na tafsiri ya sheria hizi.

(b) Miaka 5 mpaka 17	Bure	5.00
(c) Umri chini ya miaka 5	Bure	Free

**B: ADA YA KUPIGA KAMBI KATIKA PORI LA AKIBA,
ENEO LA JAMII LA KUHIFADHI WANYAMAPORI**

(1) PORI LA AKIBA NA ENEO LA JAMII LA KUHIFADHI WANYAMAPORI

(a) Ada katika eneo la kambi

Umri	Kiwango cha chini cha ada kwa mtu mmoja kwa siku moja	
	Raia Shilingi za Kitanzania	Mgeni Dola za kimarekani
(a) Miaka 18 na zaidi	5,000.00	30.00
(b) Miaka 5 mpaka 17	2,000.00	15.00
(c) Chini ya miaka 5	Bure	Bure

(b) Ada kwa eneo maalumu/kambi ya muda

Umri	Kiwango cha chini cha ada kwa mtu mmoja kwa siku moja	
	Raia Shilingi za Kitanzania	Mgeni Dola za Kimarekani
(a) Miaka 18 na zaidi	3,000.00	20.00
(b) Miaka 5 mpaka 17	2,000.00	10.00
(c) Chini ya miaka 5	Bure	Bure

(2) ENEO LA WAZI

(a) Ada kwa eneo lenye kambi

Umri	Kiwango cha chini cha ada kwa mtu mmoja kwa siku moja	
	Raia (Shilingi za Kitanzania) Kwa masaa 24	Mgeni (Dola za Kimarekani) Kwa masaa 24
(a) Miaka 18 na zaidi	Bure	25.00
(b) Miaka 5 mpaka 17	Bure	15.00
(c) Chini ya miaka 5	Bure	Bure

(b) Ada kwa eneo maalumu/kambi ya muda

Umri	Kiwango cha chini cha ada kwa mtu mmoja kwa siku moja	
	Raia (Shilingi za Kitanzania) Kwa masaa 24	Mgeni (Dola za Kimarekani) Kwa masaa 24
(a) Miaka 18 na zaidi	Bure	20.00
(b) Miaka 5 mpaka 17	Bure	10.00

Onyo: Sheria hizi zimetafsiriwa na JMT (Jumuiko la Maliasili Tanzania) – na siyo tafsiri ya kiofisi ya serikali. JMT haitahusika na uharibifu au usumbufu wowote utakaowapata au utakao mpata muhusika ye yote kutokana na tafsiri ya sheria hizi.

(c) Chini ya miaka 5	Bure	Bure
----------------------	------	------

C: ADA KWA UANDAAJI WA FILAMU AU UPIGAJI PICHA ZA SINEMA KATIKA PORI LA AKIBA, ENEO LA JAMII LA KUHIFADHI WANYAMAPORI NA ENEO LA WAZI

B: ADA YA UANDAAJI WA FILAMU AU UPIGAJI PICHA ZA SINEMA

(ii) Ada ya uandaaji wa filamu/upigaji picha za sinema

Kipindi cha utekelezaji	Ada kwa mtu mmoja kwa siku moja	
	Raia Dola za Kimarekani	Mgeni Dola za Kimarekani
Siku 1 mpaka siku 89	50.00	200. 00
Siku 90 mpaka siku 179	40.00	150.00
Siku 180 mpaka siku 720	30.00	100.00

* Ada ya uandaaji wa filamu/upigaji wa picha za cinema inahusisha gharama za kiingilio, kupiga kambi na ada ya uandaaji wa filamu yenye.

D: ADA YA GARI, BOTI ZA MASHINE, KUENDESHA CHELEZO, MTUMBWI NA SAFARI ZA KUTEMBEA KATIKA PORI LA AKIBA NA ENEO LA JAMII LA KUHIFADHI WANYAMAPORI NA ENEO LA WAZI.

(i) Ada ya gari

Aina ya uzito	Kiwango chaa chini cha ada ya kuingilia (malipo kwa siku moja)	
	Usajili wa ndani	Usajili wa nje
	Shilingi za Kitanzania	Dola za Kimarekani
Uzito wa Kg 2,000	5,000.00	5.00
Uzito kati ya Kg 2,000 – 3,000	10,000.00	10.00
Uzito kati ya Kg 3,000 – 7,000	15,000.00	20.00
Uzito kati ya Kg 7,001-10,000	20,000.00	30.00

(ii) Ada ya boti za mashine

Kiingilio cha boti/ada ya uendeshaji wa boti kwa siku	Usajili wa ndani Shilingi za Kitanzania	Usajili wa nje Dola za Kimarekani
Nguvu ya mashine ya boti (5-15 HP)	10,000.00	20.00
Nguvu ya mashine ya boti (16-45 HP)	20,000.00	30.00
Nguvu ya mashine ya boti (45 –	30,000.00	40.00

Onyo: Sheria hizi zimetafsiriwa na JMT (Jumuiko la Maliasili Tanzania) – na siyo tafsiri ya kiofisi ya serikali. JMT haitahusika na uharibifu au usumbufu wowote utakaowapata au utakao mpata muhusika yeoyote kutokana na tafsiri ya sheria hizi.

50*)		
------	--	--

- Boti zenyе nguvu ya mashine zaidi ya 50 HP haziruhusiwi

(iii) Ada ya kuendesha Chelezo/Mtumbwi

Kundi	Kiwango cha chini cha ada ya kila siku kwa kundi (Katika dola za Kimarekani)
Mtu 1 mpaka 5	200.00
Zaid ya watu 5	300.00

(iv) Ada ya safari za kutembea

Kundi	Kiwango cha chini cha ada kinacholipwa kwa kundi kwa siku moja	
	Raia Shilingi za Kitanzania	Mgeni Dola za Kimarekani
Mtu 1 mpaka watu 5	Bure	30.00
Watu kati ya 6-10	Bure	100.00

(v) Ada ya kuendesha gari ili kuangalia wanyama usiku

Umri	Kiwango cha chini cha ada kinacholipwa kwa mtu mmoja kwa siku moja	
	Raia Shilingi za Kitanzania	Mgeni Dola za Kimarekani
Watoto (Miaka 5 mpaka 17)	20,000.00	50.00
Watu wazima (Miaka 18 na zaidi)	50,000.00	100.00

(vi) Ada ya uvuvi wa kimichezo/burudani katika pori la akiba na eneo la jamii la kuhifadhi wanyamaporı.

Aina ya haki ya mtumiaji	Kiwango cha chini cha ada kinacholipwa kwa mtu mmoja	
	Raia Shilingi za Kitanzania	Mgeni Dola za Kimarekani
Kuvua na kuacha samaki (kwa siku)	10,000.00	50.00
Kuvua na kuondoka na samaki (kwa samaki mmoja)	5,000.00	10.00

E: ADA YA UONGOZAJI KATIKA PORI LA AKIBA NA ENEO LA JAMII LA HIFADHI YA WANYAMAPORI

(h) Ada kwa muongozaji aliyeajiriwa na Serikali

Onyo: Sheria hizi zimetafsiriwa na JMT (Jumuiko la Maliasili Tanzania) – na siyo tafsiri ya kiofisi ya serikali. JMT haitahusika na uharibifu au usumbufu wowote utakaowapata au utakao mpata muhusika ye yote kutokana na tafsiri ya sheria hizi.

Aina ya shughuli	Minimum fees (daily rate per guide)	
	Raia Shilingi za Kitanzania	Mgeni Dola za Kimarekani
Kuendesha gari usiku ili kuangalia wanyama	30,000.00	40.00
Kutembea/kuendesha boti/chelezo/safari za mtumbwi	25,000.00	25.00

(ii) Ada kwa waongozaji wenye taaluma

Taaluma/Ada ya usajili ya mwongozaji	*Kiwango cha chini cha ada kwa siku	**Kiwango cha chini cha ada kwa mwaka
Raia (Shilingi za Kitanzania)	20,000.00	500,000.00
Mgeni (Dola za Kimarekani)	30.00	5,000.00

*Muongozaji ambaye siye mwajiriwa wa kambi/nyumba ya kulala wageni/hoteli ambayo ipo katika pori la akiba, eneo la jamii la kuhifadhi wanyamapor ni eneo la wazi.

**Muongozanja ambaye ni mwajiriwa wa kambi/nyumba ya kulala wageni/hoteli ambayo ipo katika pori la akiba, eneo la jamii la kuhifadhi wanyamapor ni eneo la wazi.

(iii) Ada kwa waongozaji wa asili (wenyeji)

Ada kwa waongozaji wa asili (wenyeji)	Kiwango cha chini cha ada kwa siku	Kiwango cha chini cha ada kwa mwaka
Raia (Shilingi za Kitanzania)	1,000.00	10,000.00

F: ADA YA KURUSHA NDEGE NA PUTO KUBWA KATIKA PORI LA AKIBA NA ENEO LA JAMII LA HIFADHI LA WANYAMAPORI

(i) Ada ya kutua kwa ndege

Uwezo wa ndege	Kiwango cha chini cha ada cha kutua ndege (pamoja na helikopta)	
	Usajili wa ndani (Shilingi za Kitanzania)	Usajili wa nje Dola za Kimarekani
Abiria 1 mpaka 4	15,000.00	50.00
Abiria 5 mpaka 12	20,000.00	100.00
Abiria 13 au zaidi	30,000.00	200.00

(ii) (a) Ada ya uendeshaji wa puto kubwa

Kipindi cha utekelezaji	Ada kwa kipindi cha utekelezaji (Dola za Kimarekani)
Mpaka siku 90	3,000.00
Mpaka siku 180	6,000.00
Mpaka siku 360	9,000.00

Onyo: Sheria hizi zimetafsiriwa na JMT (Jumuiko la Maliasili Tanzania) – na siyo tafsiri ya kiofisi ya serikali. JMT haitahusika na uharibifu au usumbufu wowote utakaowapata au utakao mpata muhusika yeoyote kutohana na tafsiri ya sheria hizi.

(ii) (b) Ada kwa urushaji wa puto kubwa

Uwezo wa puto kubwa	Ada ya urukaji kwa mtu mmoja (Dola za Kimarekanis)
Mpaka abiria 4	50.00
Abiria kati ya 5 mpaka 12	40.00
Abiria 13 au zaidi	30.00

G: ADA YA KUHIFADHI WANYAMAPORI NA ADA YA HAKI YA MTUMIAJI KATIKA MAENEKO YA WAZI NJE YA HIFADHI ZA TAIFA, ENEO LA HIFADHI LA NGORONGORO NA MAPORI TENGEFU

(i) Ada ya kuhifadhi wanyamapor

Aina	Ada kwa mtu mmoja kwa usiku mmoja (Dola za Kimarekani)
Kambi ya mahema/nyumba ya kulala wageni	15

- Licha ya gharama zingine zilizolelezewa, ada ya uhifadhi ya dola za Kimarekani 15 kwa mtu mmoja kwa siku itatozwa pindi unapoingia katika pori tengefu.
- Kiwango cha chini cha kuweka pesa ziipatazo dola za Kimarekani 25,000.00 kama ada ya uhifadhi ambazo hazitarejeshwa kitalipwa kwa Mkurugenzi wa wanyamapor kwa niaba ya maeneo ya jamii ya utunzaji wa wanyamapor na mamlaka ya serikali za mitaa. Ada itagawanywa kutohana na kanuni za uchangiaji gharama.

** Malipo mengine na taratibu za malipo mengine ni kama ilivyo kwenye makubaliano ya mkataba kati ya mamlaka husika na mwekezaji.

(ii) Ada ya haki ya mtumiaji wa wanyamapor katika bustani ya wanyama, mashamba ya wanyama, ranchi za wanyamapor, maeneo ya utunzaji wa wanyamapor, na maeneo mengine yenye hadhi sawa (bila kuwepo na wanyama wafuata: simba, chui, kifaru, kiboko, nyati, tembo, nyoka mwenye sumu na wadudu)

Aina ya matumizi	Malipo ya ada ya haki ya mtumiaji (katika dola za kimarekani) kwa mwaka
Bustani ya wanyama	1,000.00
Mashamba ya wanyamapor na maeneo mengine yenye hadhi sawa	1,200.00
Maeneo ya utunzaji wa wanyamapor	1,500.00
Ranchi za wanyamapor	2,000.00

/
(iii) Ada ya haki ya mtumiaji wa wanyamapor katika bustani ya wanyama, mashamba ya wanyama, ranchi za wanyamapor, maeneo ya utunzaji wa wanyamapor na

Onyo: Sheria hizi zimetafsiriwa na JMT (Jumuiko la Maliasili Tanzania) – na siyo tafsiri ya kiofisi ya serikali. JMT haitahusika na uharibifu au usumbufu wowote utakaowapata au utakao mpata muhusika yejote kutokana na tafsiri ya sheria hizi.

maeneo mengine yenye hadhi sawa (ikijumuisha kati ya wanyama wafuatao: simba, chui, kifaru, kiboko, nyati, tembo, nyoka mwenye sumu na wadudu)

Aina ya matumizi	Malipo ya ada ya haki ya mtumiaji (katika dola za kimarekani) kwa mwaka
Bustani ya wanyama	2,000.00
Mashamba ya wanyamaporini na maeneo mengine yenye hadhi sawa	2,500.00
Maeneo ya utunzaji wa wanyamaporini	3,000.00
Ranchi za wanyamaporini	4000.00

(iv) **Ada ya haki ya mtumiaji wa wanyamaporini katika bustani ya wanyama, mashamba ya wanyama, ranchi za wanyamaporini, maeneo ya utunzaji wa wanyamaporini na maeneo mengine yenye hadhi sawa (yakiwa pamoja na ndege, wanyama wanaotambaa na/au wadudu)**

Aina ya matumizi	Malipo ya ada ya haki ya mtumiaji (katika dola za kimarekani) kwa mwaka
Bustani ya wanyama	1,000.00
Mashamba ya wanyamaporini na maeneo mengine yenye hadhi sawa	1,200.00
Maeneo ya utunzaji wa wanyamaporini	1,500.00
Ranchi za wanyamaporini	2,000.00

Dar es Salaam
.....2007

JUMANNE A. MAGHEMBE
Waziri wa Maliasili na Utalii